



Article History
Received: 2026.08.11
Accepted: 2026.09.07
Published: 2026.10.13

Issue no: 01 | Vol no: 07 | October 2026: 156-166

Nafasi ya Emoji katika Kujenga Maana za Kipragmatiki katika Diskosi za Kidijitali za Kiswahili

Nicholas Owino Agull ⁽¹⁾
Raphael Mwaura Gacheiya ⁽²⁾
Mark Odawo Anjejo ⁽³⁾

(1,2) Egerton University, Kenya. (3) Rongo University, Kenya.
Main author's email: Owino.14662831@egerton.ac.ke

Cite this article in APA

Agull, N. O., Gacheiya, R. M., & Anjejo, M. O. (2026). Nafasi ya emoji katika kujenga maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. *Editon consortium journal of Kiswahili*, 7(1), 156–166.
<https://doi.org/10.51317/pt5cpp81>

Ikisiri

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa emoji katika ujenzi na ufasiri wa maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Ingawa matumizi ya emoji yameongezeka katika mawasiliano ya mitandao ya kijamii, bado haijalezewa kwa makini namna emoji zinavyoashiria msimamo wa mwasilishaji, kuimarisha kauli, kupunguza au kuongeza utata na kutekeleza matendo ya usemi kwa kuzingatia muktadha na dhamira ya mtumaji. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Umuhimu ya Sperber na Wilson (1995) na kutumia muundo wa kimaelezo. Data kuu zilijumuisha emoji 285 za aina 11 zilizokusanywa kimakusudi kutoka katika diskosi za Kiswahili kwenye WhatsApp na X. Aidha, washiriki 50 waliteuliwa kimakusudi ili kufasiri na kuthibitisha maana za emoji kulingana na muktadha. Data za ziada zilikusanywa kwa kutumia dodoso, mahojiano na majadiliano ya makundi lengwa. Emoji 285 zilitumika katika uchanganuzi mkuu, huku maoni ya washiriki yakisaidia ufasiri wake. Data zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yalionyesha kuwa maana za emoji hujengwa kupitia mwingiliano wa vipengele vya kiisimu, kiutamaduni, kisemiotiki, kiteknolojia na kimwingiliano. Emoji zilibainika kuashiria mtazamo na dhamira ya mwasilishaji, kuimarisha au kurekebisha nguvu ya kauli, kutekeleza matendo ya usemi na kuelekeza ufasiri kulingana na muktadha. Utafiti huu unachangia uelewa wa emoji kama rasilimali za kipragmatiki na kutoa msingi wa tafiti zijazo kuhusu uchakataji wa lugha asilia kwa kutumia akili unde na maendeleo ya lugha za Kiafrika katika teknolojia ya kisasa.

Maneno muhimu: Diskosi za kidijitali, emoji, ishara za kidijitali, mitandao ya kijamii, pragmatiki.



This article is distributed under the license of a [Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/). It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.



UTANGULIZI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa emoji katika ujenzi na ufasiri wa maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano, husan katika mitandao ya kijamii, yamebadilisha namna watu wanavyotumia lugha kuwasiliana. Mawasiliano ya kidijitali hutegemea zaidi lugha ya maandishi, hali inayopunguza baadhi ya viashiria visivyo vya maneno vinavyopatikana katika mawasiliano ya ana kwa ana, kama toni ya sauti, sura ya uso na ishara za mwili. Kutokana na hali hii, emoji zimekuwa amali muhimu ya mawasiliano ya kidijitali kwa kusaidia kuwasilisha hisia, mtazamo, dhamira na mwelekeo wa ujumbe. Pia huathiri namna mpokeaji anavyotambua na kutathmini maudhui ya ujumbe, hivyo kuwa rasilimali zinazoshiriki katika ujenzi na ufasiri wa maana (Riordan, 2017).

Katika muktadha huo, pragmatiki ina nafasi muhimu katika kueleza namna maana ya ujumbe inavyopatikana katika matumizi halisi ya lugha yenye emoji. Maana ya kipragmatiki katika utafiti huu ilirejelea maana inayojengwa kutokana na matumizi ya lugha na emoji katika muktadha maalumu wa mawasiliano, tofauti na maana ya kisemantiki au ya moja kwa moja inayohusishwa na neno, tungo au ishara yenyewe. Maana ya kipragmatiki hujitokeza kupitia uhusiano kati ya ujumbe na muktadha, ukiwamo dhamira ya mwasilishaji, maarifa ya pamoja, uhusiano wa washiriki, mazingira ya mawasiliano na matarajio ya mpokeaji. Hivyo, maana ya emoji haiwezi kufasiriwa kwa kuzingatia umbo au maana yake ya msingi pekee, bali lazima ihusishwe na matini na mazingira ya matumizi. Dainas na Herring (2021) walieleza kuwa kazi za emoji hutegemea muktadha wa diskosi, kwani emoji huweza kutekeleza kazi tofauti kulingana na mazingira ya matumizi.

Kwa mtazamo huu, emoji ni vidokezo vinavyoelekeza namna ujumbe unavyokusudiwa kufasiriwa. Utafiti huu haukuzichunguza kama alama zenye maana moja ya kudumu, bali ulizingatia maana inayojengwa kupitia mwingiliano wa emoji, matini ya Kiswahili na muktadha wa mawasiliano. Li na Yang (2018) walibainisha kuwa emoji hutekeleza kazi mbalimbali za kipragmatiki katika mawasiliano ya mtandaoni, zikiwamo kuwasilisha hisia, kusisitiza mtazamo na kusaidia kurekebisha maana ya ujumbe. Kwa msingi huo, utafiti huu ulitathmini namna emoji zilivyoshiriki katika kuashiria dhamira ya mwasilishaji, kuonyesha mtazamo, kuelekeza au kurekebisha toni ya ujumbe, kuimarisha au kupunguza

nguvu ya kauli, na kuwasilisha maana ya kihisia. Kazi hizi zilichunguzwa kama maana zinazojengwa katika muktadha mahususi, si kama maana za kudumu za emoji. Aidha, emoji zinaweza kushiriki katika utekelezaji na urekebishaji wa vitendo vya usemi. Herring na Ge-Stadnyk (2024) walionyesha kuwa emoji huweza kuambatana na tungo za maandishi, kurekebisha maana zake au kutumika kama mchango unaojitegemea katika mwingiliano wa kidijitali. Kwa hiyo, zinaweza kuhusishwa na vitendo vya kimawasiliano kama kuomba, kuomba msamaha, kusisitiza, kukubaliana, kukataa, kusalimia au kuonyesha mtazamo. Hivyo, utafiti huu ulizingatia pia namna emoji zinavyohusiana na vitendo vya usemi na kuathiri ufasiri wa ujumbe.

Katika diskosi za kidijitali za Kiswahili, emoji zimekuwa sehemu ya mazoea ya kawaida ya mawasiliano katika nyanja za kijamii, elimu, biashara na burudani. Watumiaji huzichanganya na Kiswahili ili kuongeza taarifa za kimawasiliano na kuwasilisha maana ambazo wakati mwingine haziwezi kubainika kikamilifu kupitia maandishi pekee. Kiaer (2023) alibaini kuwa matumizi ya emoji katika mitandao ya kijamii huathiriwa na mazingira na madhumuni ya mawasiliano. Kwa hiyo, matumizi yake katika Kiswahili yalichunguzwa kama sehemu ya mabadiliko yanayotokana na mazingira mapya ya kiteknolojia na kimawasiliano.

Muktadha wa mawasiliano ni muhimu katika kuelewa nafasi ya emoji katika ujenzi wa maana ya kipragmatiki. Ufasiri wake huathiriwa na mfuatano wa mazungumzo, dhamira ya mwasilishaji, uhusiano wa washiriki, maarifa ya pamoja na mazingira ya kijamii na kiteknolojia. Kwa msingi huo, emoji zilichukuliwa kama vidokezo vya kipragmatiki vinavyomsaidia mpokeaji kutambua namna ujumbe ulivyokusudiwa kueleweka. Maana yake, hivyo, hujengwa kupitia mwingiliano wa emoji, lugha na muktadha, badala ya kutegemea ishara yenyewe pekee. Pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya emoji, bado kuna haja ya kuelewa kwa kina namna zinavyoshiriki katika kujenga na kuongoza ufasiri wa maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili.

Ingawa Riordan (2017), Li na Yang (2018), Dainas na Herring (2021), Kiaer (2023), pamoja na Herring na Ge-Stadnyk (2024) wameonyesha umuhimu wa emoji katika mawasiliano ya kidijitali, bado kuna haja ya kuchunguza katika muktadha mahususi wa Kiswahili namna emoji, matini na mazingira ya mawasiliano vinavyoingiliana katika kujenga maana. Hasa, haijalelezwa kwa kina

namna maana ya kipragmatiki inavyojitokeza katika matumizi ya emoji katika diskosi za Kiswahili na jinsi mpokeaji anavyotumia taarifa za kimatini na kimuktadha kufikia ufasiri unaokusudiwa.

Pengo hili lilishughulikiwa kwa kuchunguza namna emoji zinavyodhihirisha msimamo wa mwasilishaji, kubainisha nia ya ujumbe na kupunguza au kuondoa utata kwa kuhusisha vipashio vya diskosi. Kwa kufanya hivyo, utafiti ulilenga kuonyesha nafasi ya emoji katika kujenga maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Aidha, ulitathmini namna emoji zinavyoshirikiana na matini ya Kiswahili na muktadha ili kuunda maana inayozidi maana ya moja kwa moja ya maneno au ishara, na kupanua uelewa wa pragmatiki ya Kiswahili katika mazingira ya kidijitali.

MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti mbalimbali zimetambua emoji kama rasilimali muhimu za kimawasiliano katika diskosi za kidijitali. Dresner na Herring (2010) walieleza kuwa emoji hutekeleza kazi zinazozidi uwasilishaji wa hisia, huku Danesi (2016) akizichukulia kama mfumo mpana wa lugha ya picha katika mawasiliano ya mtandaoni. Gawne na McCulloch (2019) walizihusisha na ishara za mwili katika mawasiliano ya ana kwa ana, na Li na Yang (2018) wakaonyesha kuwa emoji huashiria hisia na mitazamo, kuimarisha au kurekebisha nguvu ya kitendo cha usemi, kuonyesha ucheshi na kejeli, na kusaidia usimamizi wa zamu za mazungumzo. Kwa pamoja, tafiti hizi zinaonyesha kuwa emoji huongeza taarifa zinazokosekana katika matini na kushiriki katika kuwasilisha hisia, mitazamo na dhamira ya mtumaji.

Hata hivyo, hazijaeleza kwa kina namna emoji zinavyoshiriki katika ujenzi wa maana ya kipragmatiki katika muktadha mahususi wa matumizi. Kinadharia, tafiti hizo hazikufafanua vya kutosha uhusiano kati ya emoji, matini, muktadha na dhamira ya mtumaji katika kumwezesha mpokeaji kufikia maana iliyokusudiwa. Kwa mtazamo wa Nadharia ya Umuhimu, pengo hili linahusu kutokuwepo kwa maelezo ya kutosha kuhusu namna emoji zinavyoathiri athari tambuzi na juhudi za uchakataji, kwa kuzingatia taarifa za kimuktadha na maarifa ya awali ya mpokeaji. Hivyo, ingawa tafiti zilizotangulia zimeainisha kazi za kimawasiliano za emoji, hazijatoa maelezo ya kutosha kuhusu mchakato ambao emoji, matini na muktadha hushirikiana katika ujenzi na ufasiri wa maana ya kipragmatiki. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza nafasi ya

emoji katika ujenzi wa maana ya kipragmatiki katika diskosi za kidijitali.

Dainas na Herring (2021) walibainisha kuwa emoji hutekeleza kazi za kipragmatiki katika mawasiliano ya mtandaoni kwa kubadili au kusawazisha toni ya ujumbe na kuelekeza namna unavyopaswa kueleweka. Hata hivyo, utafiti wao haukueleza kwa kina jinsi emoji zinavyoshirikiana na matini, muktadha na dhamira ya mtumaji katika kujenga maana mahususi, wala namna mpokeaji anavyotumia taarifa za kimuktadha na maarifa ya awali kufikia ufasiri wa ujumbe. Kinadharia, utafiti huo haukufafanua vya kutosha mchakato wa kiakili unaomwezesha mpokeaji kuhusianisha emoji, matini, muktadha na dhamira ya mtumaji, kwa kuzingatia dhana za Nadharia ya Umuhimu kama athari za kimuktadha, athari tambuzi na juhudi za uchakataji. Hivyo, licha ya kubainisha kazi za kipragmatiki za emoji, uliacha pengo kuhusu namna dhana hizo zinavyoweza kueleza ujenzi na ufasiri wa maana za kipragmatiki. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kuchanganua uhusiano kati ya emoji, matini ya Kiswahili, dhamira ya mtumaji na muktadha katika ujenzi na ufasiri wa maana ya kipragmatiki.

Utegemezi wa maana ya emoji kwa muktadha ulijadiliwa na Wijeratne na wenzake (2017), walioonyesha kuwa maana za emoji hubadilika kulingana na mazingira ya matumizi. Grosz, Greenberg na wenzake (2023) waliunga mkono hoja hii kwa kuonyesha kuwa emoji zinaweza kuchukuliwa kama vipashio vya maana vinavyokaribia hadhi ya leksimu au kama picha na ishara za kiaikoni, ambazo ufasiri wake hutegemea pragmatiki na muktadha. Hata hivyo, tafiti hizi hazikueleza kwa kina, kinadharia, jinsi maana inayokusudiwa ya emoji inavyojitokeza kutokana na mwingiliano wa emoji, matini, dhamira ya mtumaji, maarifa ya mpokeaji na muktadha wa mawasiliano.

Hivyo, kuna pengo la kinadharia kuhusu mchakato wa kiakili na kimuktadha unaomwezesha mpokeaji kufikia maana inayokusudiwa, hasa pale maana ya msingi ya emoji haitoshi kueleza tafsiri katika matumizi mahususi. Aidha, uhusiano huu haujaelezwa vya kutosha katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hilo kwa kutumia mtazamo wa kipragmatiki unaozingatia kuwa, ingawa emoji inaweza kuwa na maana ya msingi inayotambulika na watumiaji wengi, maana inayokusudiwa hubadilika kulingana na muktadha; hivyo, kuchunguza jinsi emoji, matini,

dhamira ya mtumaji, maarifa ya mpokeaji na muktadha vinavyoingiliana katika ujenzi na ufasiri wa maana ya kipragmatiki.

Gacheiya (2025) alionyesha kuwa matumizi ya Kiswahili katika majukwaa ya kidijitali yameibua ruwaza bunifu za lugha, zikiwamo emoji, vifupisho na lugha mseto, zinazorahisisha mawasiliano na kujenga utambulisho wa kijamii. Pia alibainisha kuwa matumizi hayo huathiriwa na tofauti za kitabaka na kizazi, hivyo kuhusisha vipengele vya kidijitali na mazingira ya kijamii. Ingawa utafiti wake uliweka msingi wa kuelewa Kiswahili cha kidijitali, haukuchanganua kwa kina namna emoji zinavyoshiriki kujenga na kuongoza maana za kipragmatiki.

Kwa mtazamo wa kinadharia, haukufafanua vya kutosha uhusiano wa emoji na muktadha, nia ya mtumaji, maarifa ya mpokeaji na mchakato wa ufasiri, wala namna Nadharia ya Umuhimu inavyoweza kueleza mchango wa emoji katika ujenzi wa maana kwa kuzingatia athari za kimuktadha, athari za kiakili na juhudi za uchakataji. Pengo hili ndilo lililolengwa na utafiti huu, uliolenga kueleza mchakato ambao emoji, kwa kushirikiana na matini na muktadha, hujenga na kuongoza ufasiri wa maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili, na hivyo kuendeleza mjadala kuhusu pragmatiki ya Kiswahili na matumizi ya lugha katika mazingira ya teknolojia.

Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Umuhimu iliyoasisiwa na Sperber na Wilson (1995). Nadharia hii inaeleza kuwa mawasiliano ya binadamu huongozwa na matarajio ya mpokeaji kupata ujumbe wenye umuhimu. Kwa mtazamo huu, maana ya emoji haitegemei umbo lake pekee, bali hujengwa kupitia uhusiano wake na matini, muktadha na maarifa ya mpokeaji. Nadharia hii ilitumika kuchanganua sababu za mtumaji kuchagua emoji fulani, muktadha unaomwezesha mpokeaji kuifasiri, athari za kimuktadha zinazotokana na matumizi yake, juhudi za kiakili zinazohitajika katika ufasiri, na namna mpokeaji anavyobaini maana iliyokusudiwa. Hivyo, emoji inaweza kuimarisha, kubadilisha au kuongeza maana ya matini, na wakati mwingine kuifanya itafsiriwe kama kejeli au dhihaka. Kwa jumla, nadharia hii ilitoa msingi wa kueleza uhusiano kati ya emoji, matini, muktadha, dhamira ya mtumaji na ufasiri wa mpokeaji katika ujenzi na uwasilishaji wa maana katika diskosi za kidijitali za Kiswahili.

MBINU ZA UTAFITI

Uchunguzi huu ulitumia muundo wa kimaeezo kwa kuwa ulilenga kuchunguza na kufafanua nafasi ya emoji katika kujenga maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Muundo huu ulichunguza matumizi halisi ya emoji katika mazingira yake ya asilia kwa kuzingatia muktadha wa mawasiliano. Data zilikusanywa kutoka katika diskosi za Kiswahili za *WhatsApp* na *X* kwa kutumia usampulishaji wa kimakusudi, ambapo ujumbe wenye emoji uliteuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Aidha, taarifa za nyongeza zilikusanywa kupitia dodoso na mahojiano ya kina yaliyohusisha wataalamu wa mawasiliano.

Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Umuhimu ya Sperber na Wilson (1995) kwa kuwa ilitoa msingi wa kushughulikia pengo la kinadharia kuhusu namna emoji zilivyoshiriki katika ujenzi na ufasiri wa maana za kipragmatiki. Ingawa tafiti zilizotangulia zimeeleza matumizi ya emoji katika kuwasilisha hisia, mitazamo, toni na dhima mbalimbali za kimawasiliano, bado kuna upungufu wa maelezo yalidhihirisha jinsi emoji huingiliana na matini na muktadha ili kumwezesha mpokeaji kufikia maana iliyokusudiwa na mtumaji. Hivyo, pengo si ukosefu wa tafiti kuhusu emoji, bali ni upungufu wa maelezo ya kinadharia kuhusu uhusiano kati ya emoji, matini, muktadha, dhamira ya mtumaji na ufasiri wa mpokeaji katika ujenzi wa maana ya kipragmatiki katika diskosi za Kiswahili za kidijitali.

Nadharia ya Umuhimu ilitumika kufafanua mawasiliano kama mchakato wa urejelezi ambapo mpokeaji huunganisha taarifa iliyotolewa na mtumaji na muktadha pamoja na maarifa aliyonayo ili kufikia ufasiri uliokusudiwa. Katika utafiti huu, emoji ilichukuliwa kama sehemu ya taarifa ya kimawasiliano iliyoweza kuathiri ufasiri wa matini ya Kiswahili. Kwa msingi huo, dhamira ya mtumaji huwakilisha maana au athari aliyokusudia kuwasilisha, huku mpokeaji akitumia matini, emoji, muktadha na maarifa yake kujenga fasiri iliyolingana na dhamira hiyo. Kwa hiyo, nadharia hii ilichunguza si kile emoji kilichowakilisha pekee, bali namna ilivyomwelekeza mpokeaji katika kufasiri ujumbe mzima.

Katika uchanganuzi, dhana ya Umuhimu ilitumika kubainisha mchango wa emoji katika kufikia ufasiri uliokusudiwa kwa kuzingatia uwiano kati ya athari za kimuktadha na juhudi za kiakili zilizohitajika katika kuchakata taarifa. Hivyo, emoji ilichanganuliwa kwa

kuangalia iwapo iliongeza au kuisisitiza maana, kupunguza utata, kubadili mwelekeo wa ufasiri au kumsaidia mpokeaji kutambua dhamira ya mtumaji. Kwa mfano, emoji iliifanya kauli ya Kiswahili ifasiriwe kama mzaha, kejeli, pongezi, huzuni, shukrani au onyo kulingana na muktadha.

Dhana ya muktadha ilitumika kuchunguza taarifa zilizozunguka ujumbe na kumwezesha mpokeaji kufikia fasiri iliyokusudiwa. Muktadha ulijumuisha matini iliyotangulia au kufuatia emoji, mada ya mazungumzo, uhusiano wa washiriki, maarifa ya pamoja na mazingira ya mawasiliano ya kidijitali. Kwa msingi huo, maana ya emoji haikuchukuliwa kuwa ya kujitegemea, bali hutokana na mwingiliano wake na matini na mazingira ya matumizi. Hivyo, emoji moja iliweza kufasiriwa kwa namna tofauti katika miktadha tofauti.

Dhana ya athari za kimuktadha ilitumika kubainisha matokeo ya kimaana iliyotokana na mwingiliano wa emoji, matini na muktadha. Uchanganuzi uliangalia iwapo emoji iliongeza maana mpya, kuimarisha maana iliyopo, kupunguza ukali wa kauli, kubadili fasiri, kuondoa utata au kuashiria mtazamo na dhamira ya mtumaji. Kwa hiyo, emoji haikuchukuliwa kama pambo la ujumbe, bali kama kipengele kilichoweza kuathiri uelewaji wa ujumbe na kuzalisha maana ya kipragmatiki ambayo huenda isingepatikana kutokana na matini pekee.

Dhana ya juhudi za kiakili ilitumika kuchunguza kiwango cha uchakataji kinachohitajika ili mpokeaji ahusishe emoji, matini, muktadha na maarifa yake na kufikia tafsiri inayokusudiwa. Emoji inayotoa dokezo lililo wazi inaweza kurahisisha uelewaji, ilhali emoji yenye maana tegemezi au isiyo wazi inaweza kuhitaji uhusishaji mpana zaidi wa muktadha na maarifa ya pamoja. Dhana hii hivyo ilisaidia kueleza tofauti za ufasiri wa emoji miongoni mwa wapokeaji au katika mazingira tofauti ya mawasiliano.

Kwa msingi huo, Nadharia ya Umuhimu iliunda mnyororo wa kinadharia ulioanzia katika dhamira ya mtumaji, iliyojidhihirisha kupitia matini na emoji, kisha kuchakatwa na mpokeaji kwa kutumia muktadha, na hatimaye kuzalisha athari za kimuktadha kwa kiwango fulani cha juhudi za kiakili. Mchakato huu ulionyesha kuwa maana ya kipragmatiki haipo katika emoji pekee, bali hujengwa kupitia mwingiliano wake na vipengele vingine vya mawasiliano. Hivyo, nadharia hii ilitoa msingi wa kuziba pengo la utafiti kwa kueleza jinsi emoji

zilivyomwelekeza mpokeaji kutoka kwenye matini na muktadha hadi kwenye tafsiri ya dhamira ya mtumaji.

Kwa hiyo, uchanganuzi haukuishia kubainisha aina na matumizi ya emoji, bali ulihusisha kila emoji na matini, muktadha, dhamira ya mtumaji, athari za kimuktadha na juhudi za kiakili zilizohusika katika ufasiri wake. Njia hii ilibainisha namna emoji zilivyoshiriki katika kujenga na kufasiri maana za kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili.

MATOKEO NA MAJADILIANO

Ufasiri na Uundaji wa Maana za Emoji Kimatumizi

Utafiti uliochanganua sampuli 285 za emoji kutoka aina 11 katika data za WhatsApp na X ulibaini kuwa maana ya emoji iliundwa kupitia mwingiliano wa emoji, vipashio vya kiisimu, dhamira ya mtumaji na muktadha wa mawasiliano. Matokeo yalionyesha kuwa emoji moja inaweza kuwa na maana tofauti kulingana na mazingira ya matumizi. Hivyo, maana ya emoji haikuwa ya kudumu, bali ilijengwa kimatumizi na kimuktadha, jambo linaloendana na Yus (2014) na Levinson (1983). Muktadha wa diskosi ulijitokeza kuwa kipengele muhimu katika ufasiri wa emoji. Uchanganuzi ulionyesha kuwa maana ilibadilika kulingana na taarifa iliyozunguka ujumbe, uhusiano wa washiriki na mazingira ya mawasiliano. Kwa mfano, “Umefanya vizuri sana 😊” inaweza kueleweka kama pongezi, mzaha au kejeli kutegemea muktadha. Matokeo haya yanaunga mkono Dainas na Herring (2021), wanaosisitiza umuhimu wa muktadha katika ufasiri wa emoji.

Aidha, dhamira ya mtumaji ilibainika kuwa na mchango mkubwa katika uundaji wa maana. Emoji zilitumika kuwasilisha maana ambazo hazikutajwa moja kwa moja, kama furaha, kejeli, tutoridhika, mshangao na mshikamano. Kwa mfano, “Sawa 😞” inaweza kuashiria tutoridhika licha ya neno “sawa” kuonyesha kukubaliana. Hivyo, mpokeaji alihitaji kuunganisha maneno, emoji na muktadha ili kubaini maana iliyokusudiwa, kama inavyoelezwa na Sperber na Wilson (1995).

Matokeo pia yalionyesha kuwa emoji zilitumika kuimarisha au kutekeleza matendo ya usemi kama kupongeza, kuomba msamaha, kushukuru, kuonyesha huruma na kukubaliana. Mifano kama “Hongera sana 🙌”, “Pole 🙏” na “Sawa 👍” inaonyesha uhusiano

huo. Vilevile, emoji zilitumika kupunguza ukali wa kauli, kuonyesha ukaribu na kulinda uhusiano wa kijamii, kama katika “Samahani 😊” na “Asante sana ❤️”. Hivyo, ufasiri wake ulitegemea uhusiano kati ya emoji, kauli na muktadha. Uchanganuzi ulionyesha pia kuwa emoji zilitoa vidokezo vya kufasiri kauli na kwamba maarifa ya pamoja ya kijamii na kiutamaduni yaliathiri maana zake. Kwa mfano, 🤖 inaweza kutumiwa kuashiria kicheko kikubwa badala ya maana yake ya msingi ya kifo. Hali hii inaonyesha kuwa matumizi ya mara kwa mara yanaweza kuibua maana mpya au zinazokaribiana na maana za kileksika, kama wanavyoeleza Cohn na wenzake (2023).

Kwa jumla, matokeo yalibaini kuwa uundaji wa maana za emoji kipragmatiki ulitokana na mwingiliano wa muktadha wa kiisimu, kijamii, kiutamaduni na kiteknolojia. Vipengele vilivyojitokeza zaidi ni muktadha, dhamira ya mtumaji, maana iliyodokezwa, tendo la usemi, uhusiano wa kijamii na maarifa ya pamoja. Mifano iliyotolewa ni ya kubuniwa kwa madhumuni ya kufafanua matokeo, si dondoo za moja kwa moja kutoka WhatsApp au X.

Maana ya Emoji katika Muktadha wa Kiisimu

Utafiti wa makala hii ulibaini kuwa maana ya emoji hujengwa na kufasiriwa kwa kuzingatia uhusiano wake na vipashio vya kiisimu, kama vile maneno, virai, vishazi na sentensi, pamoja na muktadha wa matumizi. Mtazamo huu uliendana na Nadharia ya Umuhimu ya Sperber na Wilson (1995), ambayo ilieleza kuwa mpokeaji huchanganua vidokezo vilivyopatikana katika ujumbe pamoja na taarifa za kimuktadha ili kupata fasiri yenye umuhimu mkubwa kwa kutumia juhudi ndogo ya kiakili. Kwa mfano, kauli “*Umejanya vizuri* 👍” ilibainisha pongezi na kuridhishwa, ilhali “*Umejanya vizuri* 😊” ilitegemea muktadha na uhusiano wa washiriki, kuashiria kejeli au maana isiyo ya moja kwa moja. Hivyo, emoji iliimarisha maana ya kauli, ilibainisha au hata kuibadili kulingana na muktadha wa mawasiliano.

Utafiti huu ulibaini pia kwamba katika mawasiliano ya kidijitali, ufasiri haukuweza kutenganishwa na muktadha, kwa kuwa mpokeaji alitumia taarifa zilizopatikana katika mazingira ya mawasiliano ili kujenga maana iliyokusudiwa. Ujumbe wa WhatsApp “*Umejika salama* ❤️” ulitumia emoji ya moyo kuongeza hisia za upendo, kujali au ukaribu; wakati ujumbe “*Sawa* 😊” uliweza

kuonyesha kicheko, mzaha au hata kejeli, kutegemea maudhui yaliyotangulia katika mazungumzo. Vilevile, ujumbe wa X “*Hongera kwa ushindi* 🏆👏” ulionyesha namna emoji zilivyoongeza nguvu ya maana iliyowasilishwa kwa maneno. Kwa msingi huo, utafiti huu ulionyesha kuwa vipengele hivyo huingiliana na muktadha wa kiisimu na kimawasiliano katika ujenzi wa maana. Kwa hiyo, maana ya emoji haitegemei umbo lake la picha pekee, bali hujitokeza kupitia mwingiliano wa emoji, lugha, dhamira ya mtumaji, maarifa ya pamoja na muktadha wa mawasiliano, katika viwango vya kisintaksia, kisemiotiki na kisemantiki.

Maana za Emoji katika Muktadha wa Kisintaksia

Uhusiano kati ya pragmatiki na sintaksia hujitokeza kwa namna nafasi ya emoji na uhusiano wake na vipashio vya sentensi vinavyoathiri ufasiri. Kwa kuzingatia kihimili cha umuhimu cha Nadharia ya Umuhimu ya Sperber na Wilson (1995), muktadha wa kisintaksia ulitoa vidokezo vilivyomsaidia mpokeaji kufikia fasiri iliyokusudiwa, huku nafasi ya emoji ikijenga, ikipunguza au ikibadili maana kulingana na vipashio vilivyoizunguka. Kwa mfano, ujumbe wa WhatsApp “*Nimefurahi kukuona* 😊 kwenye mkutano wetu” huelekeza emoji katika fasiri chanya kupitia kitenzi nimefurahi, ilhali “😊 kwenye mkutano wetu” humlazimisha mpokeaji kutegemea zaidi muktadha, dhamira na maarifa ya pamoja.

Vivyo hivyo, tofauti ya nafasi katika “*Nimefurahi kukuona* 😊” na “😊 Nimefurahi kukuona kwenye mkutano” ilidhihirisha kuwa mpokeaji aliweza kuanza ufasiri kabla au baada ya kupata taarifa za kiisimu na kurekebisha dhana yake kadiri alivyopokea taarifa zaidi. Kwa mujibu wa Tesnière (1959), kitenzi ni kitovu kinachodhibiti mahusiano ya vipashio vingine katika sentensi; hivyo, katika diskosi zenye emoji, uhusiano huu uliweza kusaidia kuelekeza fasiri yake. Hata hivyo, taarifa ya kisintaksia pekee haitoshi, kwani mpokeaji huiunganisha na muktadha, dhamira ya mtumaji, maarifa ya pamoja na maana iliyodokezwa ili kupata fasiri inayofaa.

Maana za Emoji katika Muktadha wa Kisemiotiki

Muktadha wa kisemiotiki humwezesha mpokeaji kuhusisha emoji na maneno, alama na ishara nyingine katika ujumbe, huku maana yake ikiathiriwa na mazingira ya matumizi. Kwa mfano, “*Umechelewa tena* 😊” liliashiria kukerwa, ilhali “*Umechelewa* 😊” lilimaanisha mshangao au kutoridhika kulingana na

muktadha na uhusiano wa washiriki. Vivyo hivyo, “Sawa basi 😊” lilimaanisha kukubali kwa utulivu, wakati “Sawa basi 😞” likidokeza kutoridhika. Hivyo, muktadha, dhamira na tendo la usemi vilishirikiana katika ufasiri, ambapo emoji ilidokeza kilichomwezesha mpokeaji kufikia maana iliyodokezwa. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa tofauti za kijamii na kizazi huathiri maana ya emoji; kwa mfano, emoji 🤩 iliashiria kicheko miongoni mwa baadhi ya vijana, lakini ikahusishwa na kifo katika muktadha mwingine. Pavalanathan na Eisenstein (2016), pamoja na Opoku-Fotie na Quarcoo (2026), walionyesha kuwa matumizi na ufasiri wa emoji huathiriwa na tofauti za kijamii, kizazi na mazingira ya mawasiliano. Kwa hiyo, maana ya emoji si ya jumla wala isiyobadilika, bali hujengwa kupitia matumizi, makubaliano ya kijamii, maarifa ya pamoja na muktadha wa diskosi.

Maana za Emoji katika Muktadha wa Kiutamaduni

Utafiti wa makala hii ulibaini kuwa maana ya emoji hujengwa kupitia mwingiliano wa ishara, matini, muktadha wa mawasiliano, dhamira ya mtumaji na maarifa ya mpokeaji, kwa kuongozwa na Nadharia ya Umuhimu, mpokeaji huunganisha taarifa za ujumbe na muktadha wake wa kiutambuzi ili kupata fasiri yenye umuhimu mkubwa kwa kutumia juhudi ndogo ya kiakili. Hivyo, emoji ilionwa kama kidokezo cha kimawasiliano kilichosaidia kutambua dhamira na maana iliyokusudiwa; kwa mfano, emoji 🤝 katika “Nakutakia heri 🤝” iliashiria mshikamano au nia njema, ilhali katika “Tumekubaliana 🤝 kuhusu mpango huu” iliimarisha maana ya makubaliano.

Muktadha wa kitamaduni pia ni sehemu muhimu ya ufasiri kama vile Sun na wenzake (2023) walivyoonyesha kuwa tofauti za kitamaduni ziliweza kuathiri uchaguzi na ufasiri wa emoji. Kwa mfano emoji 🙋 iliashiria salamu, kuagana au kufunga mazungumzo kulingana na muktadha, huku 🙋 ikionyesha matumaini au kutamani mafanikio. Gawne na McCulloch (2019) walieleza kuwa emoji ziliweza kutumika kama ishara za kidijitali zilizohusiana na ishara za mwili, huku maana yake ikitegemea matumizi katika muktadha husika.

Aidha, emoji zilitেকেleza au kubadili nguvu ya tendo la usemi. Katika “Hongera kwa kazi nzuri 🙌”, emoji 🙌 iliimarisha pongezi, lakini katika mazingira ya kejeli

ilidokeza dhahaka. Vivyo hivyo, emoji 🤔 na 🤨 zilibaini maana maalumu kwa mpokeaji mwenye maarifa ya utamaduni wa Kijapani au Kichina, lakini kufasiriwa tofauti na asiye na maarifa hayo. Kwa hiyo, utambulisho na uzoefu wa kitamaduni huathiri uchaguzi na ufasiri wa emoji.

Kwa jumla, emoji 🤝, 🙌, 🙋, 🤔 na 🤨 hazikuwa maana moja isiyobadilika, bali maana zake zilijengwa kupitia mwingiliano wa emoji, matini, muktadha, dhamira ya mtumaji, maarifa ya pamoja na matarajio ya mpokeaji. Pei na Cheng (2022) walionyesha kuwa maana za emoji zilitofautiana na kulingana na makundi ya kijamii na tofauti za kiisimu na kitamaduni. Kwa hiyo, uchanganuzi wa emoji katika diskosi za kidijitali za Kiswahili zilipaswa kuzingatia vipengele hivyo ili kueleza namna mpokeaji alivyofikia maana ya moja kwa moja au fiche kwa mujibu wa Nadharia ya Umuhimu.

Maana za Emoji katika Muktadha wa Kiteknolojia

Muktadha wa kiteknolojia ni sehemu muhimu ya mazingira ya utambuzi yaliyomsaidia mpokeaji kufasiri emoji kwa kuzingatia ishara, matini, jukwaa la kidijitali, mwonekano wake na uzoefu wa mtumiaji. Kwa mujibu wa Nadharia ya Umuhimu, mpokeaji hutafuta fasiri yenye umuhimu zaidi kwa kutumia juhudi ndogo ya kiakili. Tian na Liu (2025) walitambua kuwa emoji ziliweza kuongeza, kupunguza, kupinga, kujaza au kuchukua nafasi ya taarifa ya kiisimu, hivyo kuathiri juhudi za kiakili katika ufasiri. Kwa mtazamo huo, utafiti huu ulibaini kuwa, “Nimefurahi kukuona 😊” uliibua kidokezo cha hisia chanya, ilhali “Nimefurahi kukuona 😞” lilihitaji juhudi zaidi ya kiutambuzi kutokana na kutokuwa na kidokezo cha wazi cha hisia. Kwa hiyo, emoji ziliwasilisha hisia na kusimamia uhusiano wa kimawasiliano, mbali na kuashiria hisia, kuongeza nguvu ya hisia, kurekebisha nguvu ya tendo la usemi na kuonyesha ucheshi au kejeli.

Aidha, mwonekano wa emoji ulitofautiana kulingana na jukwaa au kifaa cha mawasiliano, na tofauti hizo ziliathiri ufasiri wake. Miller na wenzake (2016) walibainisha kuwa tofauti za uwasilishaji wa emoji katika majukwaa mbalimbali ziliathiri maana na hisia zilizotambuliwa na mpokeaji. Vilevile, mazoea ya jukwaa na kanuni zisizoandikwa za jumuiya ziliathiri maana za emoji. Bai na wenzake (2019) walikubaliana kuwa tofauti za kiteknolojia na kijamii zinaweza kusababisha tofauti za ufasiri, huku O’Boyle na Doyle

(2023) wakisisitiza umuhimu wa uzoefu wa mtumiaji na ujuzi wa jukwaa katika kufikia maana iliyokusudiwa. Hivyo, emoji ilibainisha au kubadili nguvu ya tendo la usemi kulingana na muktadha, kama katika “*Umefanya vizuri* 🤝”, ambalo liliweza kuwa pongezi au kejeli. Kwa jumla, utafiti huu ulitambua kuwa maana ya emoji katika muktadha wa kiteknolojia ulijengwa kupitia mwingiliano wa emoji, maandishi, jukwaa, mwonekano wa kiteknolojia, uzoefu wa mtumiaji, dhamira ya mtumiaji, maarifa ya pamoja na mazingira ya mawasiliano. Kwa hiyo, muktadha wa kiteknolojia uliweza kupunguza au kuongeza juhudi za kiakili za ufasiri, huku pragmatiki ikieleza namna vipengele hivyo vinavyoshirikiana katika kufikia maana inayokusudiwa.

Maana za Emoji katika Muktadha wa Kimwingiliano

Utafiti huu pia ulichunguza muktadha wa kimwingiliano kama mazingira muhimu ambamo maana ya emoji hujengwa na kufasiriwa kupitia uhusiano kati ya mwasilishaji na mpokeaji, mfuatano wa ujumbe, dhamira ya mwasilishaji, majibu ya mpokeaji na maarifa ya pamoja ya washiriki. Kwa mtazamo wa pragmatiki, maana ya emoji haiwezi kutenganishwa na mchakato wa mwingiliano kwa sababu mpokeaji huitegemeza fasiri yake katika kile kilichosemwa kabla au baada ya emoji, namna mshiriki mwingine alivyoitikia na uhusiano uliopo kati ya washiriki. Mtazamo huu uliendana na Nadharia ya Umuhimu, iliyodai kuwa mpokeaji huchagua fasiri iliyompatia athari kubwa za kimuktadha kwa kutumia juhudi ndogo ya kiakili.

Kwa hiyo, emoji iliweza kuimarisha, kubadili au kudokeza maana ambayo haijabainishwa moja kwa moja katika maneno. Dainas na Herring (2021) walibainisha kuwa maana ya kisemantiki ya emoji pekee mara nyingi haitoshi kueleza maana iliyokusudiwa, kwa kuwa muktadha wa diskosi na mwingiliano wa washiriki ilichangia kwa kiasi kikubwa katika ufasiri wake. Umuhimu wa mfuatano wa ujumbe katika ujenzi wa maana ya emoji ulionekana katika mazungumzo yafuatayo:

A: Umefaulu mtihani!

B: Kweli? 🤔

Katika mazungumzo haya, emoji 🤔 ilifasiriwa kama mshangao kutokana na taarifa iliyotolewa na **A**. Kwa mtazamo wa pragmatiki, mpokeaji haifasiri emoji hiyo

kwa kujitegemea, bali huihusisha na zamu ya awali “Umefaulu mtihani!” na jibu “Kweli?”. Mfuatano huo unampa mpokeaji vidokezo vya kutosha kuhusu hali ya **B** na hivyo kupunguza juhudi za kiakili zinazohitajika kufikia maana. Hata hivyo, katika kauli “Umenikamata 🤔”, emoji hiyo iliashiria aibu, butwaa au hali ya kutokuwa tayari, kutegemea mazingira ya mazungumzo. Hivyo, maana ya 🤔 hujitokeza kutokana na mwingiliano kati ya ishara yenyewe na muktadha wa kimawasiliano unaoizunguka. Muktadha wa kimwingiliano uliweza pia kuathiri maana ya emoji kupitia majibu ya washiriki na mfuatano wa zamu za mazungumzo. Kwa mfano:

A: Umefanya kazi yote mwenyewe?

B: Ndiyo 😊

A: Ahaa, sasa nimeelewa 😊

Katika mazungumzo haya, emoji 😊 haikuashiria tu hali ya furaha, bali ilidokeza hali ya kujiamini, kujigamba au maana ya kimafumbo. Jibu la **A** “Ahaa, sasa nimeelewa 😊” lilidokeza maana ya ziada kilichomwezesha mpokeaji kutambua maana iliyodokezwa na **B**. Kwa hiyo, maana ya emoji ilijengwa kupitia mnyororo wa mwingiliano, ambapo kila zamu ya mazungumzo hutoa taarifa iliyosaidia kufasiri zamu iliyofuata. Kwa mtazamo wa pragmatiki, mchakato huu ulionyesha kuwa maana fiche ya emoji iliweza kutambuliwa kutokana na uhusiano kati ya kauli, emoji na mwitikio wa mshiriki mwingine. Aidha, emoji iliweza kutekeleza tendo la usemi au kusimama kama mchango kamili wa kimawasiliano katika mwingiliano. Herring na Ge-Stadnyk (2024) wanaonyesha kuwa emoji zinaweza kurekebisha maana ya tungo ya maandishi, kutumika zenyewe kama mchango wa kimawasiliano au kuhusishwa na vitendo vya usemi vinavyotekelezwa na washiriki. Kwa mfano:

C: Samahani kwa nilichokufanyia.

D: 🙏

Katika mazingira haya, emoji 🙏 ilifasiriwa kama kukubali ombi la msamaha, kusamehe, kuonyesha unyenyekevu au kuomba msamaha zaidi, kutegemea historia ya mazungumzo na uhusiano wa washiriki. Kwa hiyo, emoji yenyewe haitoshi kutoa fasiri kamili; maana yake hukamilishwa na kauli ya awali ya **C** pamoja na maarifa ya washiriki kuhusu tukio linalozungumziwa.

Hapa pragmatiki inaonyesha kuwa emoji iliweza kuwa tendo la kimawasiliano lililotegemea muktadha ili kutambuliwa kwa usahihi. Vilevile, muktadha wa kimwingiliano uliweza kupunguza au kuongeza nguvu ya kauli. Kwa mfano:

C: Umechelewa tena.

D: Samahani 😊

Katika mfano huu, emoji 😊 inaweza kupunguza ukali wa tendo la kuomba msamaha kwa kuonyesha aibu, kujisitiri au hali ya kutokuwa na raha. Kinyume chake:

C: Umechelewa tena.

D: Samahani 🙏

Katika mazingira hayo, 🙏 iliashiria kukerwa, hasira au hisia za kulazimishwa kuomba msamaha. Kwa hiyo, maneno “Samahani” yalibaki yaleyale, lakini emoji ilibadilisha athari ya kipragmatiki ya kauli. Hali hii ilionyesha kuwa emoji ziliweza kutumika kama virekebishi vya toni vilivyomsaidia mpokeaji kutambua mtazamo wa mwasilishaji. Kwa kuzingatia dhana ya juhudi za kiakili, mfuatano wa mazungumzo ulipunguza hitaji la mpokeaji kutafuta taarifa za ziada ili kufikia maana. Kwa mfano, emoji 😊 ilipotumwa peke yake ilidhihirisha fasiri kadhaa, kama vile aibu, wasiwasi, kicheko cha kujisitiri au hali ya kutokuwa na raha. Hata hivyo, ikitumiwa katika mfuatano kama “Nilisahau kutuma faili 😊” kauli hiyo ilitoa taarifa ya kiisimu iliyopunguza utata na kumsaidia mpokeaji kuhusisha emoji na hali ya aibu au kujisitiri.

Kwa jumla, muktadha wa kimwingiliano una nafasi ya msingi katika ujenzi na ufasiri wa maana ya emoji, kwa kuwa huunganisha mfuatano wa zamu za mazungumzo, majibu ya washiriki, dhamira ya mwasilishaji, uhusiano wa kijamii na maarifa ya pamoja. Kwa mtazamo wa pragmatiki, mpokeaji hachanganui emoji kama picha yenye maana iliyokamilika, bali huihusisha na taarifa nyingine zilizopatikana katika mazingira ya mawasiliano ili kutambua maana iliyokusudiwa. Kwa kuzingatia Nadharia ya Umuhimu, mchakato huu humwezesha mpokeaji kuchanganya taarifa inayotolewa na emoji na taarifa inayopatikana katika muktadha ili kupata athari

zinazofaa kwa kutumia juhudi ndogo ya kiakili. Kwa hiyo, emoji kama 🙏, 😊, 🙏 na 😊 zinaweza kupata maana tofauti katika mazungumzo tofauti kwa sababu maana yake hujengwa kupitia mwingiliano wa emoji, lugha, mfuatano wa mazungumzo, dhamira ya mwasilishaji, mwitikio wa mpokeaji na muktadha wa kimawasiliano, jambo linalodhihirisha mchango muhimu wa pragmatiki katika ufasiri wa emoji katika diskosi za kidijitali.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Utafiti huu umebaini kuwa emoji ni rasilimali muhimu ya kipragmatiki katika diskosi za kidijitali za Kiswahili. Matokeo yameonyesha kuwa emoji huweza kudhihirisha msimamo na mtazamo wa mwasilishaji, kupambanua nia ya ujumbe na kusaidia kuondoa uwezekano wa utata katika ufasiri. Aidha, maana ya emoji hujitokeza kupitia uhusiano wake na vipashio vya diskosi, hususan matini, muktadha na dhamira ya mwasilishaji. Hivyo, emoji hazipaswi kutazamwa kama alama zenye maana ya kudumu, bali kama vidokezo vya kipragmatiki vinavyoshirikiana na vipashio vingine vya diskosi katika kujenga na kuelekeza maana inayokusudiwa.

Mapendekezo: Utafiti unapendekeza tafiti zijazo zichunguze matumizi na ufasiri wa emoji katika majukwaa mbalimbali ya kidijitali, makundi tofauti ya kijamii na lugha nyingine za Kiafrika ili kubaini tofauti za kiisimu, kijamii na kiutamaduni. Aidha, tafiti zijazo zinaweza kuhusisha akili unde na uchakataji wa lugha asilia katika kuunda mifumo inayoweza kufasiri emoji kwa kuzingatia muktadha wa kisintaksia, kisesantiki na kipragmatiki. Mifumo hiyo inaweza kuchangia katika kuboresha fasiri ya mashine, uchanganuzi wa hisia, uchanganuzi wa diskosi na teknolojia za lugha za Kiafrika. Kwa hiyo, emoji zinapaswa kutambuliwa kama rasilimali muhimu ya lugha-dijitali, na si mapambo ya ujumbe, katika utafiti wa pragmatiki na nyanja nyingine za isimu.

MAREJELEO

- Bai, Q., Dan, Q., Mu, Z., & Yang, M. (2019). A systematic review of emoji: Current research and future perspectives. *Frontiers in Psychology*, 10, Article 2221. <https://doi.org/10.3389/fpsyg.2019.02221>
- Cohn, N., Engelen, J., & Schilperoord, J. (2019). The grammar of emoji? Constraints on communicative pictorial sequencing. *Cognitive Research: Principles and Implications*, 4, Article 33. <https://doi.org/10.1186/s41235-019-0177-0>
- Dainas, A. R., & Herring, S. C. (2021). Interpreting emoji pragmatics. In C. Xie, F. Yus, & H. Haberland (Eds.), *Approaches to Internet pragmatics: Theory and practice* (pp. 107–144). John Benjamins Publishing Company. <https://doi.org/10.1075/pbns.318.04dai>
- Danesi, M. (2016). *The semiotics of emoji: The rise of visual language in the age of the Internet*. Bloomsbury Academic.
- Dresner, E., & Herring, S. C. (2010). Functions of the nonverbal in CMC: Emoticons and illocutionary force. *Communication Theory*, 20(3), 249–268. <https://doi.org/10.1111/j.1468-2885.2010.01362.x>
- Gacheiya, R. M. (2025). Kiswahili katika TEHAMA: Tafsiri kama daraja la upatikanaji wa maarifa. *East African Journal of Swahili Studies*, 8(2), 425–437. <https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3865>
- Gawne, L., & McCulloch, G. (2019). Emoji as digital gestures. *Language@Internet*, 17. <https://scholarworks.iu.edu/journals/index.php/li/article/view/37786>
- Grosz, P. G., Greenberg, G., De Leon, C., & Kaiser, E. (2023). A semantics of face emoji in discourse. *Linguistics and Philosophy*, 46(4), 905–957. <https://doi.org/10.1007/s10988-022-09369-8>
- Herring, S. C., & Ge-Stadnyk, J. (2024). Emoji and illocutionarity: Acting on, and acting as, language. In M. Gill, A. Malmivirta, & B. Wårvik (Eds.), *Structures in discourse: Interaction, adaptability, and pragmatic functions* (pp. 124–155). John Benjamins Publishing Company. <https://doi.org/10.1075/pbns.345.07her>
- Kiaer, J. (2023). *Emoji speak: Communication and behaviours on social media*. Bloomsbury Academic.
- Levinson, S. C. (1983). *Pragmatics*. Cambridge University Press.
- Li, L., & Yang, Y. (2018). Pragmatic functions of emoji in internet-based communication—A corpus-based study. *Asian-Pacific Journal of Second and Foreign Language Education*, 3, Article 16. <https://doi.org/10.1186/s40862-018-0057-z>
- Miller, H., Thebault-Spieker, J., Chang, S., Johnson, I., Terveen, L., & Hecht, B. (2016). “Blissfully happy” or “ready to fight”: Varying interpretations of emoji. *Proceedings of the International AAAI Conference on Web and Social Media*, 10(1), 259–268. <https://doi.org/10.1609/icwsm.v10i1.14757>
- O’Boyle, B., & Doyle, G. (2023). Not just iconic: Emoji interpretation is shaped by use. In *Proceedings of the 13th Workshop on Computational Approaches to Subjectivity, Sentiment, & Social Media Analysis* (pp. 452–457). Association for Computational Linguistics. <https://doi.org/10.18653/v1/2023.wassa-1.39>
- Opoku-Fofie, S., & Quarcoo, K. N. A. (2026). Semantic shift in emoji usage among Generation Z in WhatsApp group chats. *Journal of Applied Linguistics*, 5(2), 121–132. <https://doi.org/10.52622/joal.v5i2.584>
- Pavalanathan, U., & Eisenstein, J. (2016). More emojis, less :) The competition for paralinguistic function in microblog writing. *First Monday*, 21(11). <https://doi.org/10.5210/fm.v21i11.6879>
- Pei, J., & Cheng, L. (2022). Deciphering emoji variation in courts: A social semiotic perspective. *Humanities and Social Sciences Communications*, 9, Article 445. <https://doi.org/10.1057/s41599-022-01453-5>
- Riordan, M. A. (2017). The communicative role of non-face emojis: Affect and disambiguation. *Computers in Human Behavior*, 76, 75–86. <https://doi.org/10.1016/j.chb.2017.07.009>
- Sperber, D., & Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and cognition* (2nd ed.). Blackwell.

- Sun, J., Lasser, S., & Lee, S. K. (2023). Understanding emojis: Cultural influences in interpretation and choice of emojis. *Journal of International and Intercultural Communication*, 16(3), 242–261. <https://doi.org/10.1080/17513057.2022.2036790>
- Tesnière, L. (1959). *Éléments de syntaxe structurale*. Klincksieck.
- Wijeratne, S., Balasuriya, L., Sheth, A., & Doran, D. (2017). A semantics-based measure of emoji similarity. In *Proceedings of the 2017 IEEE/WIC/ACM International Conference on Web Intelligence* (pp. 646–653). Association for Computing Machinery. <https://doi.org/10.1145/3106426.3106490>
- Yus, F. (2014). *Pragmatics of Internet-mediated communication*. Peter Lang.